Dawa Inayozuilika

na

Jerry McCay

Dawa Inayozuilika

na

Jerry McCay

Novemba 5, 2011

Dawa Inayoepukika

Maswali yameulizwa kuhusu ndoa (na kutaliki) katika Kanisa tangu mwanzo wake. Muda mwingi umetumika maswali haya yakijadiliwa – baada ya kuwa tatizo. Kama ilivyo kwa ugonjwa wo wote, "awa inayoepukika" mara nyingi ni tiba nzuri. Kimsingi hii ni kweli katika swala hili. Katika jitihada za kuokoa mvutano mwingi na mioyo kuuma miongoni mwa wandugu (kuoa au kutokuoa zote hufanana), tunapenda uangalie pamoja nasi mambo kadhaa ambayo inahitajika kuzingatiwa kabla ya kuoana.

Kwanza kabisa, tunapaswa kukumbuka kwamba Mungu mara zote amekusudia kwamba watu wake waoe kulingana na mapenzi yake. Ibrahimu alitambua kwamba ilikuwa muhimu kumchagulia Isaka mwanamke aliyempendeza Bwana (Mwanzo 24:1-4; 12-14). Mustari 4, "*Bali enenda hata nchi yangu, na kwa jamaa zangu, ukamtwalie mwanangu Isaka mke.*" Akitambua hekima ya kumwomba Mungu msaada katika kumchagua mwenza wa kijana wake Yakobo, Isaka pia akamtuma kijana wake akatafute mwanamke kwa watu wake mwenyewe (Mwan. 28:1-7). Mustari wa 6, "*Usitwae mke wa binti za Kanaani.*" Kwa upande mwingine, Esau akumsikiliza baba yake, na akamwoa mwanamke ambaye hakumpendeza baba yake, wala Bwana (Mwan. 26:6-9). Samsoni pia alimchagua mwanamke aliyempendeza, lakini hakujali mapenzi ya baba yake au ya Bwana (Waamzi. 14:1-4). Mungu aliwaamuru Waisraeli wachague wanawake kutoka katika watu wake mwenyewe (Kumbu. 7:1-4). Mustari 3, "*Binti yako usimpe mwanao mume, wala usimtwalie mwanao mume binti yake. Kwa kuwa atamkengeusha mwanao mume asinifuate, ili wapate kuabudu miungu mingine; ndipo itakapowaka hasira ya BWANA juu yenu naye atakuangamiza upesi.*" (Ezra 9:2; Neh. 10:30; Neh. 13:25; Malaki 2:11). Bado Mungu anahitaji kwamba tuwachague wenza wetu kutoka katika watu wake (Wakristo). 2 Kor. 6:14, "*Msifungiwe nira pamoja na wasioamini…*". (Angalia pia Ufu. 18:4; 2 Kor. 6:17).

1 Kor. 7:39 inatuambia kwamba wajane (na Wakristo wote) wako katika uhuru wa kuoa ye yote wanayemtaka, isipokuwa tu katika Bwana. Hivyo tunaona kwamba tuko huru kuoa mshiriki ye yote wa kanisa. Kama nia yetu ya awali ni kumtumikia Bwana, na kumpendeza, basi tunatakiwa tuwachague wenza wetu kutoka katika watu wa Mungu wanaotamani kitu kama hicho.

Kama jinsi mtumishi wa Ibrahimu alivyomwomba Bwana kwa ajili ya mwongozo kwa Isaka katika kumchagua mke, nasi pia tunahitaji tuombe msaada wa Mungu tunapojiandaa kutafuta wenzetu (Mwan. 24:10-14). Yakobo 5:16, "*Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na*

kuombeana mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii." Tunatakiwa kuuliza mtu muhimu sana katika maisha yetu kutusaidia kumpata mtu muhimu wa pili katika maisha yetu. Baada ya kuongea na Bwana tunapaswa kusikiliza majibu yake, na kutafuta katika neno lake. Yer. 29:13, "*Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.*" Tunapaswa kumchunguza mtu huyu kulingana na neno la Mungu. Mtu huyu atasaidia au atazuia kutembea kwangu kwa Kikristo? Mtu huyu anaujasiri kuongea na Mungu kila siku? 1 Thes. 5:17-18, "*Ombeni bila kukoma.*". Fil. 4:6, "*… katika kila jambo kwa kusali… haja zenu zijulikane na Mungu.*" Je mtu huyu anachunguza maandiko kila siku? Je watajifunza na wewe? 2 Tim. 2:15, "*Jionyeshe kuwa umekubaliwa na Mungu mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, huku ukilitumia kwa halali neno la kweli.*" Mdo. 17:11, "*Waliyachunguza maandiko kila siku…*" Je mtu huyu anamtumikia Bwana kila mara? Mshumaa wa mtu huyu utaungana na wako ili kutoa mwanga mkali? Mat. 5:16, "*Nuru yenu na iangaze mbele za watu wapate kuyaona matendo yenu yaliyo mema, wamtukuze Baba yenu wa mbinguni.*" Je watakutia moyo kila siku katika kazi yako kwa Bwana (Yak. 1:23-25)? Tunapaswa kumchagua mtu ambaye siyo msikiaji msahaulifu, bali MTENDAJI wa neno. Je mtu huyu atakusaidia uwalee watoto wako kwa njia nzuri? "*… katika adabu na maonyo ya Bwana.*"? (Efe. 6:4; Mith. 22:6). Mtu huyu atafundisha maneno ya Bwana? "*… kwa bidii na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo?*" (Kumb. 6:7). Watoto wanajifunza kwa mifano. Mtu unayemtazamia ana tabia ambazo watoto wako watachukua? Mtu unayemchagua anaridhika kubaki mwana katika Kristo, au wanayatamani maziwa ya neno la Mungu ili kwamba waweze kukua? (1 Pet. 2:2; 2 Pet.3:18).

Marafiki, ndoa ni maamuzi ya pili muhimu ambayo tunatakiwa tufanye. Sawa na jinsi ambavyo hatuwezi kukubali kuoana na mtu kutoka katika dunia, na kuwafanya washiriki wa kanisa, hatuwezi kutarajia kumwoa mtu ambaye ni vugu vugu na kuwafanya kuwa Wakristo. Tunatakiwa tuwafanye waenda mbinguni. Mwenza tunayemchagua aidha atasaidia au atazuia katika kuyafikia malengo haya.

Ndugu na Dada, tukiwa tayari katika kumchagua mwenza kwa maisha ya awali, tunatakiwa tuwe makini, kwa msaada wa Mungu, tumchague mtu mmoja bora kutusaidia kupata uzima wa milele.

Imeandikwa kwa upendo, kwa shauku kwamba wote tuweze kupata uzima wa milele.

Jerry McCay